JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA TABORA

Namba za simu:
Mkuu wa Shule 0767636986
M/Mkuu wa Shule 0784206561
Malezi 0757464141

SHULE YA SEKONDARI MILAMBO
S.L.P 356
TABORA.
TAREHE …….

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi.
……
S.L.P ……
……

YAH: <u>MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MILAMBO HALMASHAURI YA MANISPAA TABORA MKOA TABORA MWAKA 2022/2023</u>

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka 2020/2021 tahasusi ya ……. Shule ya Sekondari Milambo ipo umbali wa kilomita moja magharibi mwa mji wa Tabora usafiri wa Taxi/Pikipiki/Bajaji unapatikana katika kituo cha mabasi mjini Tabora nauli ni Tshs. **Muhula wa masomo unaanza tarehe ……. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti Shuleni tarehe …….. Mwisho wa kuripoti ni tarehe …….**

2. **Mambo muhimu ya kuzingatia: -**
   2.1 SARE YA SHULE
   (a) Sare ya Shule ni Suruali mbili (2) nyeusi za kitambaa zenye linda mbili na pindo chini (turn up) **(suruali chini ziwe na upana wa 17 au 18**) , nyuma iwe na mfuko mmoja ,zisiwe za kubana mwili (vimodo) iwe yenye kugusu kiatu na Mashati mawili (2) meupe ya mikono mirefu.
   (b) Sare ya michezo ni jezi ya bluu na bukta au track suit ya bluu.
   (c) Viatu ni vyeusi vya kufunga na Kamba vyenye visigino vifupi (flat shoes).
   (d) Soksi jozi mbili nyeusi.
   (e) Mkanda wa kuvalia suruali mweusi wa ngozi (**Mkanda wa begi hauruhusiwi)**
   (f) Sweta dark blue yenye kola ya V
   (g) Tai nyeusi mbili
   (h) T-shirt mbili (2) rangi cream **(angalia mwisho sample mwisho**) yenye kola nyeupe

   NB. Mwanafunzi harusiwi kuja na nguo za nyumbani kwani atakuwa anashindia sare za shule (tisheti na suruali nyeusi).

2.2 ADA NA MICHANGO YA SHULE:

(a) Ada ya shule Kwa mwaka ni Tshs. **70,000/=.** Unaweza kulipa Shilingi **35,000/=** kwa muhula au kulipa ada yote kwa mara moja. Fedha hizo zilipwe kwenye Akaunti ya Shule Na. **51001100069** katika Benki ya NMB (**tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip na sio jina la mzazi). Jina la akaunti ya shule andika Milambo secondary school**

(b) Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni: -

i. Shilingi 25,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani
ii. Shilingi 20,000/= kwa ajili ya Taaluma
iii. Shilingi 30,000/= kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine.
iv. Shilingi 10,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza tu,
v. Fedha ya tahadhari 5,000/= **(haitarejeshwa).**
vi. Kitambulisho 6000/=
vii. Nembo 2000/=
viii. Mock kidato cha tano 20,000/=

MICHANGO MINGINE WEKA KWENYE AKAUNTI NA. 51001100132 NMB Jumla ya ada (70,000 kwa mwaka au 35000 kwa mhula) na michango (118,000) kwa kila mwanafunzi.

NB: Pesa taslimu hazipokelewi shuleni kabisa. Lipa kwenye akaunti husika kabla ya kufika shule.

(c) Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta shuleni ni:

i. Rimu moja kila mhula.
ii. Vitabu vya tahasusi husika kulingana na mchepuo wake.
iii. Dissecting kit kwa wanafunzi wa Biolojia kwa ajili ya mazoezi.
iv. Scientific calculator(kikokotozi) kwa wanafunzi wa hesabu na sayansi
v. Godoro 2.5 x 6 ft
vi. Shuka Jozi 2 rangi ya bluu bahari na chandurua 1
vii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe visiwe vya plastiki.
viii. Ndoo mbili ndogo (Lita kumi kila moja)
ix. Kila mwanafunzi aje na fyekeo moja, mfagio wa ndani (soft bloom) mfagio wa nje (chelewa lenye mti), water squeezer (mfagio wa kudekia) na jembe lenye mpini isipokuwa;
    a) Tahasusi ya PCM leta reki badala ya water squeezer.
    b) Tahasusi ya PCB na CBG leta hard bloom badala ya soft bloom.
    c) Tahasusi ya PGM leta Koleo badala ya jembe

3. **SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII:**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa mara baada ya kuripoti shuleni.

a. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla, ni jambo la lazima.
b. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule ni muhimu.
c. Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (Preparation).
d. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f. Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
g. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa kufanya hivyo.
h. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

4. **MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

1. Wizi
2. Makosa ya kitaluma kama vile kutokufanya mitihani, kukwepa vipindi na makosa yanafanana na hayo
3. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku tisini (90) bila taarifa/ utoro
4. Kugoma na ama kuhamasisha mgomo
5. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi mwenzake, mwalimu / mlezi na jamii kwa ujumla.
6. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote.
7. Kufuga ndevu
8. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya
9. Uvutaji wa sigara
10. Uasherati uhusiano wa jinsia moja au kuoa au kuolewa.
11. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
12. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
13. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni, vilabu maeneo ya kucheza kamali (playstation) n.k.
14. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.
15. Kudharau nembo za kitaifa mfano bendera ya Taifa, wimbo wa taifa n.k.
16. Kufanya jaribio lolote la kujiua kama kunywa sumu na kuficha maradhi ya hatari
17. Uhalibifu wa mali ya umma kwa makusudi
18. Kulala nje ya shule bila kibali na kukaa nje ya shule baada ya saa kumi na moja jioni.
19. Kukutwa na silaha bwenini kama vile panga jembe, kisu, kwanja (vitu vyenye ncha kali)
20. Kuwa nje ya shule bila kibali cha mkuu wa shule
21. Kwenda nje ya wilaya bila kibali kutoka mamlaka husika
22. Kugomea adhabu baada ya kukutwa na kosa.
23. Kukaidi maelekezo halali ya viongozi na walimu.

5. **VIAMBATANISHO NA FOMU MUHIMU**
    a. Fomu ya uchunguzi wa afya (medical examination form) ambazo zinajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali
    b. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi/ mkataba wa kutoshiriki katika mgom, fujo na makosa ya jinai
    c. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria na kanuni, kulipa ada, michango ya maelekezo mengine yatakayotolewa na shule

Nb **. Tafadhari soma kwa makini maelekezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu. Aidha shule ina kundi la whatsup la Walimu na wazazi kwa ajili ya kupata taarifa mbalimbali za shule kama taaluma,nidhamu,afya na mengineyo, hivyo kwa mzazi ambaye ana simu yenye whatsaap wasiliana na Mkuu wa Shule na Makamu Mkuu wa Shule ili kuweza kuungwa.**

Pia kutakuwa na mkutano wa wazazi wote kwa mwaka wa masomo kadiri ratiba ya shule itakavyoelekeza, taarifa mtaipata kwa njia ya mawasiliano!

Karibu sana katika shule ya milambo



DAUDI ABDALLAH MABELE

FOMU YA MZAZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA MAELEKEZO MENGINE YATAKAYOTOLEWA NA SHULE

Mimi……Mzazi/ Mlezi wa Mwanafunzi……

Nimesoma na kuzielewa sheria, kanuni na taratibu za shule na nimekubaliana nazo kama mzazi/ mlezi wa mwanafunzi na niko tayari kuzitekeleza sheria hizo pamoja na maelezo mengine yatakayotolewa na shule.

……

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi

SHULE YA SEKONDARI MILAMBO

A. FOMU YA MAELEKEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. Jina kamili la Mwanafunzi…….……
2. Tarehe ya kuzaliwa…….……..
3. Mzazi/ Mlezi…….……
4. Uhusiano na Mlezi……
5. Mahali anapoishi Mzazi/Mlezi, Mkoa…….……
   Wilaya ya……Mtaa/Kijiji …….……
6. Mawasiliano ya Mzazi/Mlezi…….……..
7. Kabila…….…. Dini …….……
8. Kazi ya Mzazi/Mlezi…….……
9. Wazazi wako hai au wamefariki (weka alama ya √)

   - Baba (amefariki) ( ) Baba yupo hai ( )
   - Mama (amefariki) ( ) Mama yupo hai ( )

10. Ndugu wengine wa karibu na Mzazi/Mlezi ambao wanaweza kutumika kama walezi wa mwanafunzi kama mzazi/mlezi husika hayupo.

    a. ……..… Mahali ……..No ya simu……..
    b. ……..… Mahali ……. No ya simu……..
    c. ……..… Mahali ……. No ya simu……..
    d. ……..… Mahali …… No ya simu……..
    e. WhatsApps namba ……. (kwa ajili ya taarifa na matokeo)

11. **SANDUKU LA POSTA/NAMBA YA WHATUPS LA MZAZI/MLEZI KWA AJILI YA KUTUMA MATOKEO:**
    ……
    ……
    ……

B. MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI

Mimi (Jina la mwanafunzi) …….
Nimesoma na kuelewa sheria, kanuni na taratibu zote za shule ya bweni, na niko tayari kuzitekeleza kwa muda wote nitakapokuwa shuleni hapa kama mwanafunzi. Nitakapo kiuka kipengele chochote cha shule hivyo adhabu stahili ichukuliwe dhidi yangu kwa mujibu wa sheria na taratibu.

……



Saini ya Mwanafunzi **Mkuu wa Shule**

MEDICAL EXAMINATION FORM

Medical examination form to completed by government medical officer and return to the Head master Milambo secondary school

Student full name……

Present age……..

Blood test…….…….……

Examination stool……

T.B test…….

Asthma…….……

Eye disorder……

Nose disorder……..

Ear disorder ……..

Skin disease……

Anemia……

Chest…….…….

Operations…….……

Serious Accidents…….……

Any other infections disease…….……

Additional information e.g. Physical defects or impairment, chronic or family diseases etc…….……

……

I certify that I have personally examined Mr./Miss……and found him/her fit unit to purpose studies

Signature…….

Designation…….

(Official rubber stamp) ……..

VITABU VYA REJEA (REFERRENCE BOOK)

Ni lazima na ni muhimu kwa kila mwanafunzi kuja vitabu vya masomo yake husika (angalau kimoja kwa kila somo) vitabu pendekezwa hapa chini.kila mwanafunzi azingatie vitabu kulingana na mchepuo wake wa masomo.

1. **ENGLISH LANGUAGE**
    a. A man of the people (By Chinua Achebe)
    b. The beautiful ones are not yet born (by Ayi Kwei Armah)
    c. An enemy of the people (by Henrik Ibsen)
    d. Betrayal in the city (by Francis Imbuga)

2. **BIOLOGY**
    a. Biological science (by D.J.Taylor)
    b. New understanding biology (by Susan Toole)
    c. Advanced Biology (by Michael kent)
    d. Biology – a functional approach (by M.B.V. Robert)

3. **ADVANCED MATHEMATICS**
    a. Essential for A level. pure mathematics form 6 by Telem Majigwa
    b. Essential for A level. pure mathematics form 5 by Telem Majigwa
    c. Conceptual mathematics for form 6 by Mayombya
    d. Conceptual mathematics for form 5 by Mayombya
    e. Pure understanding mathematics 1 & 2 by Backhouse
    f. S'CHANDI MATHEMATICS Volume I & II

4. **KISWAHILI**
    A. USHAIRI
        - Kimbuga – Haji Gora
        - Mapenzi Bora – Shabani Robart
        - Fungate Ya Uhuru- Mohamed S Khatibu
        - Chungu Tamu – Theobald Mvungi

    B. RIWAYA
        - Usiku Utapokwisha- Mbunda Msokile
        - Kufikirisha - Shabani Robart
        - Mfadhili – Hussein Tuwa
        - Vuta Nikuvute – Shati Adam Shati

    C. TAMTHILIA
        - Kwenye Ukingo Wa Thim –Ebrahim Hussein
        - Morani- Emmanel Mbogo
        - Kivuli Kinaishi- Said Mohamed
        - Nguzo Mama- Penina Muhando

5. **HISTORIA**
    - Morden world history 2nd edition by Ben walsh
    - Morden world history 1nd edition by Ben walsh
    - Fundamental principle of history paper 1&2 by Magoti B
    - Major events in African history by Juvitus Kamara
    - Essential in advanced history paper 1 & 2 Saleh Yassin
    - Mastering advanced level history paper 1 & 2 by Kato

6. **PHYSICS TEXT BOOKS**
    - ADVANCED LEVEL PHYSICS BY S'CHAND XI 7edition

- ADVANCED LEVEL PHYSICS BY S'CHAND XII 7edition
- ADVANCED LEVEL PHYSICS BY NELKON 7edition

7. FRENCH TEXT BOOKS

- Anne- marie niane (2002) ***L'E□NGE□RE E□dition***
- Ferdinand oyono (1956) line vie de boy
- M.M Diabat***e***□ (2002) le coiffeur de koita (Édition hatier international–paris
- Hachette (1995), dictionnaire universal 2nd edition
- A.Kon***e***□ (2002) Les frasques D' Ébirto hatier international

8. ECONOMICS TEXT BOOKS

- Introduction to economics 7edition by S.J,Grant
- Economics student guide 5edition By John Bean Shaw
- Advanced Economics theory 13edition by M.L.Jhingan
- Macro economics 2edition by David C colanders
- Economics explained .Revised 3edition by Peter Maunder

9. GEOGRAPHY TEXT BOOKS

- Geography An Integrated Approach By David Waugh
- Land Forms In Africa , By Collin Buckle
- Map Reading For East Africa By Mc Master
- Africa , A Study Geography For Advanced Students By J.M Pritchad
- Advanced Economics Theory 13edition By M.L.Jhingan
- Physical Geography In Diagrams By R.B. Bunnet
- Human and economic geography by morgan
- Research Methodology By C. Kothari

10. CHEMISTRY TEXT BOOKS

- physical chemistry (1st edition by Ngaiza)
- conceptual chemistry volume I (for class xi) s; chands)
- organic chemistry (Ngaiza)
- general chemistry with physical chemistry by (APE)
- General chemistry (Ngaiza)

TU
NGE
HIGH SCHOOL
TAIFA